# Programu ya Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Misitu (FORVAC)

## Kuendeleza Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii



The United Republic of Tanzania
MINISTRY OF NATURAL RESOURCES AND TOURISM
Forestry and Beekeeping Division

Ministry for Foreign Affairs of Finland

# Ifahamu Programu ya Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Misitu (FORVAC)

Programu ya Kuboresha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Misitu (FORVAC), imesaidia kuwepo kwa maendeleo endelevu ya rasilimali za misitu na kuhuisha mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu kwa hapa Tanzania. Programu hii ilianza mwezi Julai mwaka 2018. Programu hii inafadhiliwa na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Ufini (MFA Finland) na Wizara ya Maliasili na Utalii, Tanzania (MNRT), kupitia Idara ya Misitu na Nyuki (FBD).

FORVAC imejikita katika kuendeleza mnyororo wa mazao ya misitu hasa katika uzalishaji wa timbao, mkaa na mazao ya misitu yasiyohusiana na miti au mazao yasiyo mbao (NWFP/NTFP). Programu hii inashughulika zaidi na kutunza misitu ya asili kwa njia ya Usimamizi Shirikishi wa Jamii (CBFM) ambayo iko katika ardhi inayomilikiwa na vijiji. Kwa sababu hiyo vyanzo vya kujikimu vya jamii vitokanavyo na misitu vimeongezeka na hivyo kuchangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika maeneo ambako Programu hii inatekelezwa.

Programu hii itanufaisha watu wapatao 330,000 wakiwemo watu binafsi, jamii, vikundi vya uzalishaji, wafanya biashara, na makampuni binafsi katika mikoa ya Tanga, Lindi na Ruvuma. FORVAC pia inazisaidia asasi za serikali katika kuunda mifumo ya sheria na sera ili kuboresha utawala bora wa rasilimali za misitu na kukuza usimamizi endelevu wa rasilimali za misitu.





## Maudhui ya Programu

FORVAC inalenga katika kuongeza faida za kiuchumi, kijamii na kimazingira kutokana na misitu na kupambana na ukataji miti hovyo kwa kutekeleza yafuatayo:

1) Kuanzisha Hifadhi za Misitu ya Vijiji na kuendeleza vyanzo vya kujikimu na mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu.

2) Kuwajengea uwezo wanajamii katika vijiji vipatavyo 103 ambako programu inatekelezwa (kwa kuwapa mafunzo, zana na vitendea kazi). Kadhalika kuwajengea uwezo watendaji katika ngazi ya jamii na kati wanaohusika na utekelezaji wa Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii (CBFM) na kukuza mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu. Programu hii pia itasaidia taasisi za elimu na utafiti.

3) Kuboresha huduma za ugani, mawasiliano, ufuatiliaji na tathmini (M&E).

4) Kuendeleza na kusaidia mifumo ya kisheria na kisera inayohusiana na mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu na usimamizi endelevu wa rasilimali za misitu.

## Eneo ambako Programu ya FORVAC inatekelezwa

Makao makuu ya FORVAC yapo Dodoma lakini programu hii inatekelezwa katika kongani tatu zinazojumuisha wilaya 12 kama ifuatavyo:

- Kongani ya Tanga: Wilaya za Handeni na Kilindi mkoani Tanga, wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma na wilaya ya Kiteto (Msitu wa Jamii wa Suledo) mkoani Manyara.
- Kongani ya Lindi: Wilaya za Liwale, Ruangwa na Nachingwea.
- Kongani ya Ruvuma: Wilaya za Namtumbo, Tunduru, Songea, Mbinga na Nyasa.

Kwa ujumla FORVAC inatekelezwa katika vijiji 103 vilivyomo katika wilaya zilizotajwa.



## Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi na Usajili wa Misitu ya Hifadhi ya Vijiji katika Gazeti la Serikali

FORVAC inasaidia uhamasishaji na uanzishwaji wa misitu ya vijiji na kuhakikisha kuwa misitu hiyo inamilikiwa na vijiji kwa matumizi endelevu. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni 2021 FORVAC ilkuwa imesaidia utengenezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji 41 yenye ukubwa wa eneo la hekta 620,087 likiwemo eneo la misitu lenye jumla ya ukubwa wa hekta 158,008. Vilevile FORVAC imetengeneza Mipango ya Usimamizi wa Misitu na Mipango ya Uvunaji Misitu kwa ajili ya vijiji 32 yenye eneo la jumla ya ukubwa wa hekta 259,639. Kadhalika, misitu ya vijiji 16 imesajiliwa katika gazeti la serikali na hivyo kurasimisha umiliki wa wanavijiji wa misitu hiyo.

## Kiwango cha miti kinachoruhusiwa kuvunwa kwa mwaka

Hiki ni kiasi cha miti kinachoruhusiwa kuvunwa kwa mwaka toka katika misitu kwa malengo ya uvunaji endelevu. Viwango hivi vimefikiwa kwa umakini mkubwa katika kupitia Mipango ya Usimamizi wa Misitu iliyoandaliwa kwa msaada wa FORVAC na kufikia mwezi Juni mwishoni 2021 mipango hii iliweza kubaini mbao zenye jumla ya ujazo wa 64,774 m3 ambazo zingepatikana kupitia kiasi cha uvunaji kinachoruhusiwa. Kwa sasa kiasi cha ujazo wa mbao kilichoonyeshwa hapa kinaweza kuvunwa, kuuzwa na kuchakatwa na hivyo kuwapatia wanavijiji kipato cha uhakika na kuboresha huduma za jamii katika vijiji husika.

Jedwali hili linaonyesha kiasi cha uvunaji Kilichoruhusiwa kwa mwaka kulingana na Mpango wa Usimamizi wa Misitu uliofadhiliwa na FORVAC kwa kila eneo na wilaya husika.


| Eneo | Ruvuma | Lindi | Tanga |
|---|---|---|---|
| Wilaya | Namtumbo: 4,205m$^3$ | Ruangwa: 3,276m$^3$ | Handeni: 797m$^3$ |
| | Songea: 5,237m$^3$ | Liwale: 45,232m$^3$ | Kilindi: 1,155m$^3$ |
| | Tunduru: 1,615m$^3$ | Nachingwea: 3,258m$^3$ | |
| Jumla ya kiasi kinachoruhusiwa | **11,057m$^3$** | **51,766m$^3$** | **1,951m$^3$** |

# Mnyororo wa thamani wa mbao: Misumeno ya kisasa inayomilikiwa na wanajamii

FORVAC imenunua na kuunganisha mashine mbili za kupasua mbao zinazohamishika ambazo zinamilikiwa kwa pamoja na vijiji 28. Vijiji tisa vikiwa mkoa wa Ruvuma na 19 vikiwa mkoa wa Lindi. Mashine hizi zimeongeza tija na thamani ya mbao na hivyo kuongeza kipato cha wanajamii.

» Mashine hizi zimeongeza kiwango cha ufanisi kwa asilimia 60 ya upasuaji wa magogo ukilinganisha na ufanisi wa asilimia 30 kwa kutumia teknolojia ya kizamani na misumeno ya mikono.

» Thamani ya mbao za ujazo wa mita moja ni takriban asilimia 60 zaidi ukilinganisha na kuuza mti ambao bado haujakatwa (uliosimama).




Waziri wa Maliasili na Utalii Dr. Damas Ndumbaro akizindua rasmi mashine hizo na kuzikabidhi kwa wanavijiji katika sherehe zilizofanyika Ruvuma na Ruangwa mwezi Machi 2021.

Wanavijiji husika wamepatiwa mafunzo mahsusi ili kujenga dhana ya umiliki wa mashine hizo miongoni mwa jamii. Wamefundishwa pia kufanya matengenezo ya kawaida na matumizi salama ya mashine hizo ili ziweze kutumika kwa mafanikio. Mashine hizo zinatoa nafasi za ajira kwa vijiji vyote 28.

# Mnyororo wa thamani wa mbao: Mashamba ya mitiki/misaji na upandaji wa kurudishia miche ya miti kwenye maeneo yasiyo na miti



Wanakijiji wakishiriki katika kupanda miti.

FORVAC imesaidia kuanzisha na kuendeleza mashamba ya mitiki katika wilaya ya Nyasa iliyopo kongani ya Ruvuma. Kwa kushirikiana na vijiji vinne, FORVAC imebaini sehemu ambazo zinafaa kwa kupanda mitiki na kushirikiana na wanakijiji kuandaa mashamba kwa ajili ya kupanda miti hiyo. Katika msimu wa upandaji wa mwaka 2020 na 2021 wanavijiji wamepanda vipando vya mitiki 456,000 katika eneo la ukubwa wa hekta 409. Baadhi ya kipato cha awali kinaweza kupatikana kwa kuuza miti iliyopunguzwa, lakini ndani ya miaka ishirini kutoka sasa wananchi watapata kipato kizuri kwa kuuza miti iliyopandwa.

Wajumbe wa kamati ya maliasili ya kijiji wakishiriki upandaji miti ambao ulichukua siku tano. Usafirishaji wa miche kwenye mipaka ya misitu ulikuwa changamoto, hata hivyo wajumbe walikuwa na hamasa ya kupanda aina hiyo ya miti kwani hukua haraka na ina thamani kubwa na itakuza uchumi wa kijiji hapo baadaye



Mwezi Aprili mwaka 2021 upandaji wa kurudishia miche ya miti kwenye maeneo yasiyo na miti ulifanyika katika Msitu wa Hifadhi ya Kijiji cha Mnkonde wilayani Kilindi. Upandaji miti huo ulikuwa sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Usimamizi wa Misitu ulioidhinishwa ambapo miche 11,600 ilipandwa katika sehemu ya mipaka yenye urefu wa kilometa 13 na maeneo ambayo yaliharibiwa yenye ukubwa wa hekta 3.75.

## Mnyororo wa thamani wa mbao: Mafundi seremala vijijini wapata mafunzo ya kutengeneza mizinga ya nyuki



Mizinga ya nyuki iliyotengenezwa kwa utaalamu imekuwa ikipatikana nje ya eneo la utekelezaji wa programu ya FORVAC na imekuwa ikiuzwa kati ya shilingi 100,000/- na 120,000/- za Kitanzania. Bei hii ni ya aghali kwa wafugaji wa nyuki wa vijijini. Vipimo sahihi vya ukubwa wa mizinga, malighafi iliyo bora na mambo mengine ya kiufundi ni muhimu katika utengenezaji wa mizinga ya kisasa ili kuongeza mavuno ya mazao ya nyuki.

Ufugaji nyuki kama njia mbadala ya kujiingizia kipato, FORVAC iliwezesha mafunzo ya kutengeneza mizinga ya nyuki kwa mafundi seremala 41. Mafundi hao waliwakilisha kila kijiji ambako FORVAC inasaidia ufugaji nyuki katika wilaya za Handeni, Mbinga na Liwale. Mafunzo yalihusu utengenezaji wa mizinga ya kisasa na mizinga ya kibiashara.

FORVAC iliwapa mafundi waliohitimu mafunzo hayo tenda ya kutengeneza mizinga ya nyuki 1,544, kazi ambayo iliwapatia jumla ya shilingi 115,800,000/- za Kitanzania.

Wafugaji wa Nyuki kupitia programu ya FORVAC waliahidi kuwekeza sehemu ya mapato yao katika kuendeleza ufugaji nyuki kitu ambacho kitaenda kuwaongezea idadi ya mizinga kadri ya mpango wao wa biashara. Kutengeneza mizinga na kuiuza na kuendeleza ufugaji nyuki utanufaisha wadau wote katika siku zijazo na hivyo kuboresha uchumi wa wana jamii na kuongeza kipato kutokana na mauzo ya asali na kuwekeza kiasi cha kipato kwenye jamii kwa kununua mizinga mingine kutoka kwa mafundi seremala waliopo vijijini.



**Mafundi Seremala wa vijijini wakitengeneza mizinga ya nyuki ili kufanikisha tenda ya mizinga 1,544 waliyopewa na FORVAC.**



## Mnyororo wa thamani wa zao la asali: Kuwaunganisha wafuganyuki na wanunuzi kutoka sekta binafsi

Wafuganyuki wa wilaya za Handeni na Mpwapwa walikuwa wakipata shida ya soko la uhakika na uzalishaji mdogo wa asali yenye ubora hafifu. Wilaya zote mbili zilikuwa na uwezo wa kuboresha mnyororo wa thamani wa zao la asali hivyo FORVAC iliviunganisha vikundi 25 vya wafugaji wa nyuki na kampuni binafsi ya kununua asali, iitwayo Swahili Honey. Kampuni hiyo ina malengo ya muda mrefu ya kuwajengea uwezo wa kuinua shughuli za wafuganyuki na kuwapatia soko la uhakika la asali na nta.





Kutokana na ushirikiano huo, wafugaji wa nyuki walipewa mafunzo ya ufugaji bora wa nyuki na masuala mengine yanayohusiana na ufugaji wa nyuki, na kupewa vitendea kazi muhimu kama vile mizinga ya kibiashara, mavazi ya kujikinga na zana na kuvunia asali. Sambamba na hiari ya kuuza asali yao kwa kampuni ya Swahili Honey ambao huichakata na kuiuza kwa wanunuzi wengine.

## Kutoka mizinga isiyo na nyuki hadi kuingia nyuki kwa asilimia 100

*"Hapo awali kuna mtu alitupatia mizinga ya nyuki na kutupa mafunzo darasani. Wakati huo, tulikuwa na mizinga 30, lakini mizinga mingi haikuwa na nyuki badala yake wadudu waharibifu waliingia kwenye baadhi ya mizinga, hatukujua tufanyeje. Tulifikiri kuwa wadudu wale ndiyo waliozuia nyuki wasiingie, tukaweka dawa ya kuua wadudu kwenye mizinga yote, dawa hiyo iliua hata wale nyuki wachache waliokuwa kwenye mizinga michache. Kimsingi hatukupata chochote kutokana na shughuli ya ufugaji nyuki.*

*Hata hivyo mambo yalibadilika baada ya Afisa Ugani kutoka Swahili Honey kutufundisha namna ya kutambua aina mbalimbali za wadudu na jinsi ya kupambana nao. Alituonyesha namna ya kuwavuta nyuki kwenye mizinga kwa kumhamisha malkia kutoka kwenye mzinga mmoja na kumpeleka kwenye mzinga mpya. Sasa mizinga yetu yote imejaa nyuki.*

*Afisa Ugani wanaendelea kuja kutusaidia ili kuhakikisha kuwa nyuki wametulia na hivyo kutoa asali nyingi. Ametueleza kuwa tukipenda tunaweza kuwauzia asali yetu ili mradi iwe na ubora wa kiwango cha juu. Wako tayari kununua asali yetu kwa shilingi 70,000/- za Kitanzania kwa dumu lenye ujazo wa lita 20, pamoja na masega.*

*Huu ni mpango mzuri kwetu kwani tunaweza tukaelekeza nguvu zaidi katika kufuga nyuki na tukavuna asali nyingi kutoka katika kila mzinga. Vilevile, msimu wa kuvuna asali unaingiliana na msimu wa kuvuna mazao mashambani mwetu hivyo huwa tunakuwa na kazi nyingi, lakini shughuli ya kuvuna asali haihitaji muda mwingi.*

*FORVAC walitupatia mizinga minne ya kibiashara na 50 ya kisasa. Kwa ujuzi tulio nao tunatarajia kupata lita 20 za asali kutoka katika kila mzinga. Hii ina maana kwamba tukiendelea kushirikiana na kampuni ya Swahili Honey tunaweza kupata kati ya shilingi 5,000,000 - 6,000,000 za Kitanzania kwa mwaka. Kwa sababu hiyo tumeamua kununua mizinga kutokana na asilimia 20 ya fedha tulizopata kutokana na mauzo ya asali tuliyovuna,"* alieleza Hassani Msami, Mwenyekiti wa Kikundi cha Ufugaji Nyuki cha Kijiji cha Kwedikabu wilayani Handeni.

## Kusaidia biashara ndogondogo

FORVAC imetekeleza mradi wa majaribio wa kuwezesha biashara ndogondogo zinazohusiana na misitu katika ngazi ya kijiji katika wilaya za Handeni mkoani Tanga, Liwale mkoani Lindi na Mbinga mkoani Ruvuma. Katika kila wilaya biashara ndogondogo 20 zilichaguliwa ili kupata ufadhili. Ufadhili huo ulijumuisha kutengeneza mpango wa biashara, mafunzo na uwekezaji.

Shughuli zilizowezeshwa zilikuwa katika aina ya biashara zifuatazo:

| Aina ya biashara | Idadi ya biashara zilizofadhiliwa |
|---|---|
| Ufugaji nyuki | 30 |
| Useremala | 17 |
| Kuchuma uyoga pori, kuuchakata na kuuza | 5 |
| Kutengeneza sanaa za mikono kutokana na mianzi | 4 |
| Kuuza mianzi | 2 |
| Kutengeza majiko banifu kwa kutumia udongo mfinyanzi | 2 |

Biashara hizi zilianzishwa na jumla ya wajasiriamali 656 wakiwemo wanaume 389 na wanawake 267.

Katika kila wilaya mshauri mmoja wa biashara alifanya kazi na wajasiriamali kuanzia Oktoba 2020 hadi Agosti 2021. Ushauri ulijikita kwenye kurasimisha biashara, kutengeneza mpango wa biashara, kukokotoa faida, kutunza kumbukumbu za biashara, kutafuta masoko na kusaidia majadiliano na wanunuzi.

Katika kusaidia uwekezaji, FORVAC ilitoa malighafi, vitendea kazi na mashine mbalimbali ili kukuza biashara.

# Ushauri wa biashara uliongeza uwezo wa kujadiliana na kuboresha kiwango cha kupata faida

Kikundi cha Jitegemee kutoka kijiji cha Mazingara wilayani Handeni kinatengeneza majiko banifu kwa kutumia udongo wa mfinyanzi ambao hupatikana katika Msitu wa Hifadhi ya Kijiji. Kabla ya ushauri wa biashara haujaanza, kikundi kilikuwa na msambazaji wa bidhaa mmoja tu ambaye alikuwa Mkata mjini. Walikuwa wanamlipa malipo ya awali kama kamisheni kwa kuweka majiko hayo dukani kwake na alipata malipo halisi baada ya majiko yote kuuzwa. Kikundi kilikuwa kinapata faida ndogo sana.

Mshauri wa biashara aliona utaratibu huu haukuwa wa haki na aliwasaidia kikundi kufanya utafiti wa bei mjini Mkata. Kwa mshangao, kikundi cha Jitegemee kiliweza kupata bei nzuri zaidi kwa bidhaa zake kwani kiliweza kulipwa fedha yote mara baada ya kupeleka bidhaa kwa msambazaji bila kutanguliza malipo ya kamisheni. Sasa wakawa na nguvu ya kujadiliana na msambazaji wa awali aliyeko Mkata mjini. Hivyo kikundi cha Jitegemee wakaachana na msambazaji huyo na badala yake walipata wasambazaji wengine watatu kwa makubaliano mazuri zaidi.



## Uanzishaji wa vikundi vya kuweka akiba

FORVAC imesaidia wanavijiji kuanzisha vikundi vya kuweka na kukopa katika kongani ya Ruvuma, Lindi na Tanga. VICOBA ni vikundi vya kuweka na kukopa na husaidia kukuza biashara ndogondogo zinazohusiana na misitu katika jamii.

Jumla vikundi 11 vya VICOBA vimeanzishwa katika kongani ya Ruvuma, vikundi 8 katika kongani ya Tanga na vikundi 38 katika kongani ya Lindi. Vikundi hivi vina jumla ya wanachama 1,309 wakiwemo wanaume 509 na wanawake 800. Kwa sababu ya kuwepo vikundi hivi, watu wa vijijini wanaweza kupata mikopo yenye riba nafuu. Mikopo hii inawasaidia kukuza biashara zao na kuboresha maisha yao.



## Kupunguza umaskini kupitia VICOBA

Bi Halima Moshi mwenye umri wa miaka 27 ni mzazi mwenye mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka minne ambaye anamlea peke yake. Bi Halima anaishi katika kijiji cha Ikuyu wilayani Mpwapwa. Yeye ni mmoja wa waanzilishi 25 wa kikundi cha VICOBA kinachoitwa Mabadiliko. Kikundi hiki kilianzishwa kati ya mwezi Mei na Juni 2020 kwa masaada wa FORVAC.

Bi Halima anasimulia alivyonufaika na kikundi hiki cha VICOBA:

"Awali haikuwa rahisi kwangu kupata mkopo kwa wakopeshaji binafsi wa hapa kijijini kwasababu walikuwa wanatoza riba kubwa sana, karibu asilimia 50. Kana kwamba hiyo ilikuwa haitoshi walikuwa wanataka niweke dhamana. Ilikuwa vigumu pia kupata mkopo kutoka mabenki yaliyoko mjini Mpwawa kwani yako mbali zaidi ya kilometa 90 kutoka hapa kijijini.

Nilipojiunga na kikundi cha VICOBA mwezi Mei 2020, mambo yalianza polepole ambapo kila mwanachama alitakiwa kuweka shilingi 6,000/- za Kitanzania kila wiki. Baada ya miezi kadhaa wanachama tuliruhusiwa kukopa mara tatu ya kiasi kile ambacho mwanachmа alikuwa ameweka kwa riba ya asilimia 10.

Ilipofika mwezi Januari mwaka 2021 nilipata mkopo wa shilingi 300,000/- za Kitanzania ambazo nilitumia kununua mizinga ya nyuki ya kisasa sita kwa ajili ya manzuki yangu. Wakati huo tayari nilikuwa na mizinga minane ya asili.

Mpaka sasa mizinga ya kisasa na ile ya asili yote imeingia nyuki. Natarajia kuvuna kilo 90 za asali ifikapo mwezi Julai mwaka huu (2021) ambazo zitanipatia shilingi 900,000/- za Kitanzania kwani kilo moja ya asali huuzwa kwa shilingi 10,000/- za Kitanzania hapa kijijini. FORVAC wametuunganisha na kampuni ya Swahili Honey ambayo ina mpango wa kununua asali mbichi kutoka hapa kijijini. Hii ni kama ndoto iliyotimia na baada ya muda mfupi mimi na familia yangu tutauaga umaskini."

## Mafunzo katika ngazi ya jamii

Shirika la Mpango wa Kuhifadhi na Kuendeleza miti ya Mpingo (Mpingo Conservation and Development Initiative, MCDI) na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) wamekuwa washirika wakubwa wa FORVAC katika kuendesha mafunzo katika ngazi ya vijiji.

Washirika hawa wameboresha uwezo wa kiutawala na usimamizi wa taasisi za vijiji hasa Kamati za Maliasili za Vijiji, Halmashauri za Vijiji na Mikutano Mikuu ya vijiji.

Mafunzo haya yanahusu mada kama:


- Kujenga uelewa juu ya usimamizi Shirikishi wa Misitu, na Usimamizi wa Misitu ya Jamii
- Utawala Bora na usimamizi wa fedha za kijiji
- Tathmini Shirikishi ya Rasilimali za Misitu
- Upimaji wa magogo na mbao na ukokotoaji wa ujazo
- Usimamizi wa uvunaji



Baada ya kujengewa uwezo Kamati za Maliasili za Vijiji zimepata utaalamu wa kusimamia misitu ya vijiji kwa namna endelevu na kusimamia shughuli mbalimbali zinazohusu misitu ya vijiji. Ili kuchangia juhudi hizo FORVAC imetoa zaidi ya pikipiki 21 mpya kwa vijiji mbalimbali ili kusaidia shughuli za kamati za maliasili za vijiji.

Mamlaka za wilaya zina wajibu wa kutoa msaada unaohitajika na kijiji kila wakati. Kadhalika, FORVAC imewapatia maafisa ugani pikipiki mpya 15 ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na waweze kuwafikia wananchi kwa urahisi na kupata huduma kwa muda sahihi.

*Mratibu wa FORVAC Kongani ya Lindi, Eustack Bonifasi akikabidhi pikipiki kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Liwale.*











"Misitu endelevu - Maisha endelevu"

# ZIJUE MBINU ZA KUPATA ASALI BORA, NA KUKUZA UCHUMI WAKO KUPITIA UFUGAJI NYUKI

Tanzania ni moja ya nchi zilizoidhinishwa kuuza Asali katika mataifa ya Ulaya. Bei ya asali ya asili yenye ubora uliotibilishwa ni kubwa, na zaidi ya asilimia 90 ya ardhi ya Tanzania inafaa kwa ufugaji wa nyuki. Hivyo hii ni fursa muhimu!

1 **Weka mizinga yako mbali na mashamba ya mazao ya kilimo yanayotumia viuatilifu**



2. **Zalisha asali kwa Wingi.** Ili kuwavutia wafanyabiashara wakubwa kununua asali yako ni lazima uzalishe kwa wingi, angalau tani 20 hadi 100 kwa mwaka. Wazalishaji wadogo wanashauriwa kuunda umoja wa uzalishaji asali

3. **Hakikisha unavuna asali iliyokomaa vizuri.** Wakati wa kurina, tenganisha masega meusi na yale yenye rangi ya goldi. Asali yenye rangi ya goldi inakuwa na mvuto zaidi sokoni



4. **Uhifadhi:** Hifadhi asali katika chombo kisafi, kikavu na kisichoruhusu hewa kupita. Weka mbali na joto kali na epuka kuweka asali katika vyombo vilivyotumika kuhifadhi bidhaa nyingine kama petroli



5. **Zingatia ubora:** Zingatia kuzalisha asali yenye ladha na harufu nzuri, na kiwango kidogo cha maji. Matumizi ya moto au madawa wakati wa kurina yanaharibu sana ubora wa asali.

6. **Weka lebo yenye maelezo muhimu:** Jina, Aina ya Asali, Anuani ya mzalishaji; Chanzo cha asali mfano – mikoko, miombo, ukanda wa pwani; tarehe ya uzalishaji na uchakataji, ujazo



7. **Viwango vya Uthibitishaji;** Zingatia kuzalisha asali inayokidhi viwango vilivyowekwa kimataifa ili kupata fursa ya kuiuza nje ya nchi

8. **Wekeza katika matumizi ya teknolojia:** Zingatia matumizi ya mizinga bora, vifaa bora vya kurina, kuchakata, kuhifadhi na kusafirisha asali yako



Mizinga ya kisasa



Asali iliyokomaa



Mizinga ya kisasa



Mashine ya kuchakata asali unaotumiwa na wafugaji wadogo wa Nyuki - Tabora


**Imeandaliwa na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA)**
**kwa Ufadhili wa Mradi wa Kuongeza Mnyororo wa Thamani ya Mazao ya Misitu Tanzania**

Kwa Mawasiliano zaidi: Mkurugenzi Mtendaji; Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA);
S.L.P 21522 Dar-es-Salaam – Tanzania; tovuti: www.mjumita.org barua pepe: mjumitaorg@mjumita.org

Kwa ufadhili wa ushirikiano wa Tanzania na Finland


*MJUMITA wametengeneza vifaa vya mawasiliano ili vigawanywe kwa wanavijiji. Vifaa hivyo ni pamoja na vipeperushi na mabango. Bango la mfano hapo juu linaeleza mbinu za kuzalisha asali bora na kuboresha maisha ya wanakijiji kwa kufuga nyuki.*

# Wafadhili na Washauri

The United Republic of Tanzania
MINISTRY OF NATURAL RESOURCES AND TOURISM
Forestry and Beekeeping Division

**Wizara ya Maliasili na Utalii ni Wakala Mfadhili-Mshirika wa FORVAC, na msimamizi muhimu wa maendeleo na utekelezaji FORVAC.**
**https://www.maliasili.go.tz/**

Ministry for Foreign Affairs of Finland

**Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ndiyo mfadhili wa FORVAC na ndiyo wizara kiongozi kutoka Serikali ya Ufini.**
**https://um.fi/frontpage**

# Mshauri

Finnish Consulting Group (FCG) ni mshauri wa kimataifa katika fani mbalimbali anayetoa Ushauri wa Kiufundi kwa FORVAC.
https://www.fcg.fi/en

**Forestry and Value Chains Development Programme**
**P.O.Box 13451, Kilimani Street, 40472 Dodoma**
**www.forvac.or.tz**